**10 JUNI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Arobaini na Tatu – Tarehe 10 Juni, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa tunaendelea na Kikao cha Bunge, Mkutano wa Kumi na Tisa, Kikao cha Arobaini na Tatu.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Maswali, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Nimwite Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Temeke sasa aulize swali lake.

Na. 547

**Kuyatambua Maeneo Yote ya Maafa**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyatambua maeneo yote yanayoathiriwa na maafa na kuweka mkakati wa ziada?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Temeke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza hatua mbalimbali za kimkakati katika kuyatambua maeneo yaliyoathirika na maafa pamoja na kuweka mikakati ya muda mfupi na mrefu kupunguza athari za maafa hayo kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004, Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 6 ya mwaka 2022 pamoja na miongozo ya kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ambazo Serikali imezichukua ili kutambua maeneo yenye maafa na kupunguza madhara ya maafa hayo ni pamoja na kuandaa Wasifu wa Majanga wa mwaka 2019 ambao umeainisha maeneo yote yaliyo katika hatari; kufanya tathmini ya vihatarishi vya maafa katika Wilaya 36 na kuimairisha mifuko ya ufuatiliaji wa mwenendo wa majanga, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali; je, Jimboni kwetu Temeke hivi ninavyoongea kuna maafa, kuna sehemu ambayo ipo ndani ya Kata ya Kilakala sehemu inaitwa Bongotonyo. Tumeshaisemea sana ndani ya Serikali; je, mpo tayari sasa kuangalia au ipo ni mojawapo kati ya haya majimbo ambayo mmesema yamewekwa 36? Mpo tayari kwenda kuiangalia na je, mnatusaidiaje kwa kipindi hiki? Maana yake ni janga kubwa kwetu ndani ya Temeke pamoja na Tandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia swali la pili; upi mkakati wa Serikali wa kuongeza au kuweka fedha za ziada ndani ya mifuko hii ya maafa kabla Serikali Kuu haijaja kufanya kazi hiyo? Kwa sababu ndani ya majimbo yetu kunakuwa na maafa yanatokea, lakini fedha zinakuwa ni kidogo sana.

Je, ni upi mkakati wa Serikali kuweka fedha kidogo ndani ya majimbo yetu au wilaya zetu, ili sasa inapotokea maafa majimboni kwetu, yaanze kufanyiwa kazi kabla ya Serikali Kuu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge Dorothy Kilave kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika Jimbo lake na nieleze tu wazi na nikiri mbele ya Bunge lako siyo tu hayo maeneo anayoyataja, kuna maeneo mengine pia kwenye kata yake na ninakumbuka kwa mwaka wa fedha 2021/2022 alizungumza kwenye Kata za Kilakala, Miburani, Keko, Chamazi na maeneo mengine Mianzini na Kibondemaji, napo pia wakati wa mvua kumekuwa kukiwa na changamoto kama hizo za mafuriko ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za Serikali kwa kweli zimekuwa zikichukuliwa ikiwa ni pamoja na yeye katika ushiriki wake. Utakumbuka kwenye baadhi ya maeneo Serikali ilianza kurejesha miundombinu ya barabara, lakini pia hatua nyingine ni urejeshaji wa mifereji pamoja na hata pale kwenye maeneo ambayo yalilazimu kutengeneza shule, ili wanafunzi wasipate changamoto kwenye yale maeneo, wewe Mheshimiwa Mbunge ulikuwa sehemu ya kuhakikisha wananchi hawa huduma zinarejea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata kwenye maeneo ambayo yalihitaji vivuko, Mheshimiwa Mbunge utakumbuka kwamba tuliweka, ni moja ya jitihada za Serikali katika kuhakikisha kwamba tunakabiliana na maafa hasa ya mafuriko yanapotokea kwenye maeneo hayo ya wananchi, ili kurejesha huduma kuweza kuendelea kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hatua ya pili ameuliza swali la pili kuhusiana na mfuko kwamba uwepo mfuko. Sheria yetu hii ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004 haikuanzia sera yenyewe lakini sheria ya mwaka 2022, Sera ya 2004, sheria ya mwaka 2022 inaeleza kinagaubaga kunakuwa na Kamati za Menejimenti ya Maafa kwenye maeneo yetu na zinaanzia ngazi ya kijiji inaenda ngazi ya kata, wilaya mpaka mkoa. Kwenye haya maeneo kutokana na mapato wanayoyapata na mipango ya halmashauri ambao ndio watekelezaji wa majukumu haya na Wakuu wa Wilaya wakiwa wasimamizi wa ngazi ya Mkoa na Wilaya, inapotokea kuna changamoto yoyote inaenda kwenye bajeti zao ndani ya halmashauri na hatua ya pili ni bajeti za kimikoa kwa ajili ya maafa, lakini inapotokea kwamba jambo hili limeenda kwenye ngazi ya kuwa na maafa makubwa ya juu zaidi kuna utaratibu pia wa kutoa taarifa kwenye Kamati ya Maafa ya Taifa. Huko pia tunao mfuko ambao upo kwa mujibu wa sheria wa kushughulika na masuala ya maafa.

Kwa hiyo, ikitokea hali kama hiyo ni taarifa tu na mara nyingi Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imekuwa iki-*respond* sana kwa haraka ikiwemo kwenye jimbo lako pia hata pale Manyara utakumbuka watu wamejengewa nyumba na wanaishi vizuri. Kwa hiyo, hali hii Mheshimiwa Mbunge inapotokea Serikali ipo pamoja na wewe katika ngazi zote, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, nimuite sasa Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 548

**Kutengeneza Barabara za Zege – Same**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga barabara za vijijini zilizopo milimani - Same kwa mawe au zege ili kupunguza gharama za kufanya matengenezo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Waziri, Mheshimiwa Zainab Katimba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (NHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Same ni miongoni mwa wilaya ambazo zina mtandao wa barabara zilizoko sehemu za milimani kwenye Tarafa za Mamba, Vunta, Gonja, Chome Suji, Ndungu na Mwembe Mbaga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Serikali imekwisha jenga barabara za zege zenye urefu wa mita 5,692 kwa gharama ya shilingi bilioni 3.87 katika Barabara za Hedaru – Vunta – Myamba, *Mpirani Dispensary – Dindimo Primary School,* Maore – Vuje, Maore – Kalungoywo, Msanga – Chome, Hedaru – Makasa, Saweni – Gavao, Ndungu – Lugulu, Kisiwani – Msindo na Suji – Mweteni katika maeneo yenye kona hatarishi za mlima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2025/2026 Serikali imeweka katika mipango yake ujenzi wa barabara za zege zenye urefu wa mita 530 katika Barabara za Bombo – Mpirani, Kizangaze – Mtii, Hedaru – Vunta, Idaru – Narema, Mbuyuni – Marindi na Manka – Madiveni kwa gharama ya shilingi milioni 360.39.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuhudumia barabara na madaraja Wilayani Same kwa kujenga, kukarabati na matengenezo zikiwemo barabara zenye tabaka la zege kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana ambayo yanatia moyo. Ninashukuru sana kwamba kwenye sehemu hizi za barabara zilizotiwa zege zimeboresha sana usafiri katika kata tajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu ni kwamba; je, kwa kuwa mitaro iliyojengwa pembezoni mwa hizi barabara ziizotiwa zege, mvua ikinyesha madongo na takataka zinaangukia pale inaziba na kutembea na barabara na kuharibu yale maeneo ambayo hayajatiwa zege.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuunda kikosi kazi cha vijana ili waweze kuwa wanahudumia hizi barabara wakati *TARURA* labda hajaweza kufanya kazi hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (NHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa adui namba moja wa barabara zetu hizi ni maji na hasa sasa hivi Serikali imejielekeza katika kujenga barabara pamoja na miundombinu ya mitaro, lengo ikiwa ni ku-*drain* yale maji ili yasiharibu barabara. Sasa kuna mazingira ambayo inatokea kwamba ile mitaro inajaa takataka na lile lengo la kujengwa mitaro ile linapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI imebuni mradi mahususi kabisa kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* kwa ajili ya kuunda vikundi vya kijamii ambavyo vitakuwa na kazi mahsusi kabisa ya kufanya matengenezo madogo pamoja na kufanya usafi wa barabara zetu ikiwa ni sehemu mojawapo kwanza ya kuwasaidia vijana na haya makundi ya kijamii kupata ajira, lakini pia ikiwa ni mkakati mahususi kabisa wa kuhakikisha barabara zinazojengwa na Serikali zinaishi kwa muda uliopangwa wa kutengenezewa mazingira ya kuwa bora zaidi na kuondoa mazingira ya uchafu

kwenye mitaro, lakini maji kutwama kwenye barabara na kuziharibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali kupitia mradi huu ambao unaitwa *CDRM Component of the RISE Project* ambao huu mradi upo chini ya Benki ya Dunia kwa kushirikiana na *ILO* Serikali imeshaanza kufanya majaribio katika baadhi ya halmashauri, lakini lengo mradi huu ufike katika maeneo yote Tanzania kuhakikisha kwamba barabara zetu zinalindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa zina jukumu la msingi la kuhakikisha inafanya usafi wa mazingira katika maeneo yao.

Kwa hiyo, pia nitumie nafasi hii kuendelea kuwakumbusha Wakurugenzi wote katika Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kutimiza wajibu wao wa msingi wa kutengeneza mazingira ya usafi wa mazingira ikiwa ni pamoja na usafi katika maeneo ya miundombinu hii ya mitaro ili kuepusha mazingira ya mitaro kujaa na barabara mwisho wa siku kuharibika japokuwa miundombinu hii ya ku-*drain* maji tayari inakuwa imetengenezwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Ole-Sendeka, halafu utafuata Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Barabara ya Msitu wa Tembo kwenda Ngorika imejengwa na *TARURA* kwa kujenga tuta la kilometa mbili na kuweka lami juu sasa na kujenga madaraja; je, Serikali inasema nini kuhusu kujenga barabara hiyo kilometa kumi zilizokuwa zimeahidiwa kujengwa kwa barabara ya lami ili kuweza kuwezesha eneo hilo liweze kupitwa kwa uhakika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (NHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara zetu hizi zinazosimamiwa na *TARURA* yaani barabara za wilaya na ndio maana utaona kwamba kila mwaka wa bajeti fedha zinaendelea kuongezwa katika upande huu wa kuhudumia barabara hizi za *TARURA*. Tunazungumza mwaka 2020/2021 bajeti ya *TARURA* ilikuwa ni shilingi bilioni 275 lakini muda huu tunavyozungumza katika mwaka wa bajeti 2025/2026 tunatarajia bajeti ya *TARURA* itakuwa ni shilingi trilioni 1.18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la bajeti hii ya *TARURA* linaonekana hata katika wilaya zetu. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Ole-Sendeka kwamba Serikali kwa kuwa tayari imeshaanza kujenga hii kilometa mbili katika Barabara ya Msitu wa Tembo kwenda Ngorika, nimhakikishie hata hii kilometa kumi nyngine ya lami iliyobakia Serikali itafika, ili ihakikishe inaiboresha barabara hiyo ili iweze kuwanufaisha wananchi katika shughuli zao za kiuchumi, pia katika kufikia huduma za msingi za kijamii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, barabara inayotoka Kijiji cha Bweya kilichopo Kata ya Rwezela kwenye Jimbo la Geita haipitiki kabisa kwa sasa, si kwa gari, si kwa pikipiki. Barabara hiyo haikuwemo kwenye bajeti kwa sababu ilipewa fedha na *TASAF* kama shilingi milioni 60.

Mheshimiwa Mwenyekti, kutokana na mafuriko yaliyojitokeza kwenye Jimbo la Geita, barabara hii imeharibika kwa kiasi kikubwa na tathmini ya *TARURA* imetoka kama milioni 130. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri unatamka nini kuhusu kuiongezea fedha ya dharura barabara hiyo ili iweze kutengenezwa watoto waweze kupita kwenda shule? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (NHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuna mazingira ambayo barabara zetu hizi za *TARURA* zinakatika mawasiliano yaani mawasiliano yanakatika kutoka eneo moja kwenda linguine na ndio maana Serikali inatenga bajeti ya dharura. Katika mwaka wa bajeti huu tuliokuwa nao bajeti ya dharura ni shilingi bilioni 71 na Bunge hili lilipitisha nyongeza ya bajeti ya shilingi bilioni 50 kwa ajili ya kuhudumia eneo hili la barabara hizi ambazo zinaharibika kwa mazingira ya dharura.

Kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumuagiza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa akishirikiana na Meneja wa *TARURA* wa Wilaya waweze kuifikia barabara hii aliyoitaja Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na kuifanyia tathmini na walete maombi Ofisi ya Rais - TAMISEMI walete huku kwa *Chief* wa *TARURA,* ili tuiweke katika mipango ya kuifikia na kuihudumia kwa dharura.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara kutoka Lundugai kwenda Kambi ya Chokaa - Simanjiro kwa Mzee Sendeka hapa, haipitiki kwa sasa na hivyo mawasiliano kati ya Wilaya ya Hai na Simanjiro ni kama yamekatika kabisa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara hii muhimu ya kuunganisha wilaya hizi mbili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (NHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatammbua mazingira ambayo yanajitokeza ambapo maeneo yanaathirika na mawasiliano yanakatika kutokana na mazingira ya mvua na hali nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kumuagiza Meneja wa *TARURA* wa Kilimanjaro akishirikiana na wa

Manyara pamoja na Mameneja wa Wilaya hizi mbili wahakikishe kwamba wanafanya tathmini katika eneo hili alilolitaja Mheshimiwa Saashisha Mafuwe na waweze kuleta maombi ya fedha kwa ajili ya kuja kuchukua hatua za kidharura za kurudisha mawasiliano katika barabara hii ambayo inaunganisha Wilaya mbili za Hai na Simanjiro. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Nicholaus Ngassa.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, pale kwetu Igunga kuna mkandarasi amesaini mkataba Barabara ya kutoka Igunga Mjini kwenda Mwanzugi, itumba, Lugubu mpaka njia panda ya kule Nsimbo, lakini mpaka sasa zaidi ya miezi mitatu mkandarasi hajaingia *site* lakini ameshasaini mkataba.

Nini kauli ya Serikali kupitia TAMISEMI na *TARURA* kuhakikisha mkandarasi huyu anaingia *site,* ili aweze kutoa huduma kwa wananchi hususan ukanda huu ambao unazalisha Kilimo cha Mpunga kwa wingi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (NHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa Serikali ya Awamu ya Sita lengo lake kubwa ni kuhakikisha kwamba, inaendelea kuboresha miundombinu ya barabara zetu hizi za *TARURA,* lakini kikubwa zaidi kwa maenelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, amekuwa akisisitiza kwamba wakandarasi pindi wanapokuwa wametia saini katika mikataba kwa ajili ya kufanya kazi hizi za ujenzi wa barabara, basi waweze kusimamia makubaliano yale ambayo yapo katika mkataba ya kutekeleza mradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwagiza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Tabora, lakini na Meneja wa *TARURA* wa Wilaya, waweze kuniletea taarifa ya kwa

nini mkandarasi huyu ambaye ametia saini katika mkataba wa ujenzi wa barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge bado hajafika *site* na hajaanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kuhakikisha kwamba mkandarasi huyu anatimiza wajibu kwa mujibu wa mkataba. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tutafuatilia suala hili mimi na wewe, nitakupa mrejesho. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Barabara ya Rukuraijo kwenda Kitwechenkura mpaka kuunganisha Kata ya Songambele tumeiandikia muda mrefu; ni lini barabara hii itajengwa ili ipitike vizuri?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kuimarisha barabara zetu hizi muhimu kabisa za *TARURA*, barabara za wilaya ambazo zina umuhimu mkubwa katika kuwasaidia wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi, lakini kufikia huduma za msingi kabisa za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na utaiona dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita kuimarisha barabara hizi kwa ongezeko la Bajeti na hizo bajeti siyo tu bajeti kwa ujumla wake, lakini inaonekana hata katika ongezeko la bajeti katika kila wilaya.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Bilakwate kwamba katika barabara aliyoitaja dhamira ya Serikali ni kuifikia. Serikali itaifikia barabara hii ili iweze kuijenga na iweze kuwanufaisha wananchi wako.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa nashukuru. Tunaendelea, bado tuko Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nimwite sasa Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalumu sasa aulize swali lake.

Na. 549

**Hitaji la Uzio Shule za Mkoa wa Lindi**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga uzio kwa shule zilizopo maeneo hatarishi kwa kuwa shule nyingi za Mkoa wa Lindi hazina uzio?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya elimu nchini ikiwa ni pamoja na kujenga uzio katika shule mbalimbali za msingi kwa kuzipa kipaumbele shule zenye watoto wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2022/2023 – 2023/2024 Serikali imetoa shilingi bilioni 5.57 kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika shule 185 za watoto wenye mahitaji maalum, ikiwemo Shule ya Msingi Namakonde iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa. Aidha, shilingi milioni 105.57 zimetumika kujenga uzio katika Shule za Sekondari Lindi Wasichana na Nachingwea Wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaendelea kutenga fedha za ujenzi wa uzio kwa ajili ya usalama wa wanafunzi na mali za shule kadiri ya upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Pathan.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na kwa Serikali kuwajali watoto wetu, lakini nina ombi moja kwa Serikali. Fedha zilizopelekwa kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa shule zile ni kidogo sana, na tukiangalia Mkoa wa Lindi ni sehemu hatarishi kwa mara mbili. Hatarishi zingine zilizopo za kawaida, lakini pia

kuna hatarishi za wanyama hawa wanaitwa tembo, tembo wanatembea sana usiku kwenye maeneo yale. Nitoe ombi rasmi kwa Serikali kwa Mkoa wa Lindi, kwa shule zilizoko Mkoa wa Lindi, ni hatari sana kwa watoto wetu wanapotoka madarasani usiku na wanapokwenda kupata huduma za kijamii nje, kama kwenda *toilet*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali, tufanye mchakato huu kwa haraka kwa sababu shule zile uzio haujakamilika, ili tupate pesa hizo kwa haraka tumalizie uzio ili kuwanusuru watoto wetu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nadhani alikuwa anatoa *comment,* una cha kusema? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa Mheshimiwa Mbunge na maombi yake kama Serikali tumeyapokea. Tutaweka kipaumbele katika kuhakikisha kwamba tunajenga uzio katika shule ambazo zipo katika maeneo hatarishi, siyo tu Mkoa wa Lindi, lakini maeneo yote nchini na hasa yale maeneo ambayo yapo karibu na maeneo yenye wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari katika Mkoa wa Lindi tumeshaanza kujenga uzio kama nilivyotangulia kusema; Shule ya Sekondari ya Lindi Wasichana imejengewa uzio, *Nachingwea Girls* imejengewa uzio, Shule ya Msingi ya Namakonde imejengewa uzio na tunaendelea na kazi hiyo kufikia shule nyingine nyingi kuhakikisha na zenyewe zinajengewa uzio kwa ajili ya usalama wa wanafunzi na mali zao, lakini kwa kuhakikisha tu usalama kwa ujumla wake. Kwa hiyo, tumepokea maombi yako Mheshimiwa Mbunge na tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa nimewaona. Tuanze na Mheshimiwa Benardeta Mushashu.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya *Rugambwa Secondary* ni shule ya wasichana ya siku nyingi ambayo iko Mkoani Kagera, na kwa kuwa haina uzio shule hii inaweza ikaingiliwa na watu wabaya wakati wowote kutoka pande zote nne.

Je, ni lini Serikali itajenga na kumaliza uzio kuzunguka Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Rugambwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajenga uzio katika shule zetu hizi kwa ajili ya lengo kuu la kuhakikisha usalama wa wanafunzi, lakini mali za shule. Serikali inafanya hivyo kwa kutumia mapato ya ndani ya halmashauri, na hivyo naomba nitumie nafasi hii kuwakumbusha Wakurugenzi wa Mamlaka zile za Serikali za Mitaa kuweza kufanya tathmini katika shule ambazo ziko katika mazingira yenye mazingira hatarishi, wafanye tathmini ya gharama zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika shule hizo na kuweka katika mipango na bajeti ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kuanza kujenga uzio katika shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Benardeta Mushashu naomba ukae ukiwa na matarajio kwamba katika Shule hii ya Wasichana ya Rugambwa itajengewa uzio ili kuendelea kuimarisha usalama wa wanafunzi, lakini mali za shule. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Tunza Malapo.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwa kuwa maeneo mengi ya shule yanavamiwa na wananchi kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

Je, Serikali haioni sasa umefika wakati muafaka wanapotenga bajeti ya kujenga shule basi wanatenga na bajeti ya uzio ili shule inapokamilika inakuwa imekamilika na uzio wake kuepusha hayo mambo mengine? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, uzio ni sehemu muhimu sana ya miundombinu inayohitajika kwa ajili ya kujenga shule zetu hizi, na ni kweli kabisa Serikali inaweka msisitizo mkubwa.

Kwanza, Serikali inajenga kwa awamu, kwa hiyo, fedha tayari zinatoka kwa ajili ya kujenga miundombinu ya msingi kabisa ambayo itawezesha wanafunzi kupokelewa kwa ajili ya kuanza masomo katika shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majengo haya ya msingi kuwa yamekamilika, ni wajibu wa msingi wa Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kupitia mapato ya ndani waweze kuhakikisha wanaweka katika bajeti ya mapato ya ndani kujenga uzio. Kwa hiyo, Mheshimiwa Tunza Malapo, Serikali itaendalea na mikakati hii ya kuhakikisha kwamba kupitia fedha za mapato ya ndani ya halmashauri inafika katika shule mbalimbali kwa ajili ya kujenga uzio.

**MWENYEKITI:** Aah, niliwaona, tuanze na Mheshimiwa Dkt. Chaya, tutakwenda Mheshimiwa Chinguile, halafu Mheshimiwa Charles Kajege.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule za Sekondari za Mwanzi na Shule ya Wasichana ya Solya ambazo zipo Manyoni hazina uzio, nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba tunajenga uzio au *fence* katika shule hizi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia dhana nzima ya ugatuzi wa madaraka kutoka

Serikali Kuu kwenda kwenye Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, wajibu wa msingi wa kuweza kujenga miundombinu katika shule zetu, lakini katika sekta muhimu kabisa hizi ambazo zinagusa wananchi, ni wajibu wa Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa. Serikali Kuu inaongeza nguvu kuhakikisha kwamba pale ambapo Mamlaka zetu za Serikali za Mtaa zimefika, basi zinaongezewa nguvu katika miradi hii ya maendeleo ikiwemo katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumkumbusha Mkurugenzi wa Halmashauri hii aweze kufanya tathmini katika shule hizi ambazo amezitaja Mheshimiwa Dkt. Chaya na kubaini bajeti inayohitajika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hii ya uzio katika shule hizi, na aweke katika mipango na bajeti ambayo inatokana na mapato ya ndani kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanajenga uzio katika shule hizi kwa ajili ya kuimarisha usalama wa wanafunzi, lakini mali za shule. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chinguile.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na tunaishukuru Serikali kwa ujenzi wa shule nyingi mpya za msingi na sekondari. Ziko shule ambazo zimejengwa katikati ya makazi ya watu na hii ni kutokana na miundombinu ambayo ilishajaa tangu zamani.

Je, Serikali haioni haja sasa wakati wa ujenzi wa shule hizi ambazo ziko katikati ya makazi ya watu, ni vizuri tukapeleka na *component* ya uzio ili kuweza kulinda vijana wetu wanaosoma katika maeneo haya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Sera ya Elimu Bila Malipo udahili wa wanafunzi umeongezeka maradufu na mazingira hayo yametengeneza

uhitaji mkubwa sana wa ongezeko la miundombinu ya shule. Serikali Kuu kwa wakati huu kipaumbele chake namba moja ni kuhakikisha inajenga miundombinu ya msingi kabisa ambayo itawezesha kuanza kupokea wanafunzi hawa waweze kuanza kupata masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia na dhana hii ya *D by D* yaani ugatuzi wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye Mamlaka zile za Serikali za Mitaa, wajibu wa msingi wa kutenga bajeti na kupanga maendeleo ikiwemo kujenga miundombinu ya msingi kabisa katika sekta hizi za elimu, afya na kadhalika, ni wajibu wa Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, kazi ambayo inafanyika na Serikali Kuu ni kuongeza nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niendelee kutumia nafasi hii kuwasisitiza Wakurugenzi katika Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa waweze kufanya tathmini katika maeneo ambayo yanahitaji uzio katika shule ambazo zinahitaji uzio, lakini siyo tu shule, hata katika vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya, wafanye tathmini ya fedha inayohitajika kwa ajili ya kujenga miundombinu hiyo na waweze kuweka katika mipango na bajeti za mapato yao ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kuhakikisha wanaanza kujenga miundombinu hii muhimu kabisa ya uzio kwa ajili ya usalama wa wanafunzi au tuseme wananchi kwa upande wa Sekta ya Afya, lakini mali za shule na vituo vya afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzio wa waya katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mara iliyoko katika jimbo langu unaonekana kutokutosheleza yale mahitaji yaliyokusudiwa. Je, ni lini sasa Serikali itajenga uzio kwa kutumia matofali ili kutosheleza mahitaji tunayoyataka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kupongeza jitihada zilizofanyika katika kujenga uzio katika eneo alilolitaja Mheshimiwa Mbunge, na japo Mheshimiwa Mbunge anaeleza kwamba uzio huu haujitoshelezi na kuna uhitaji wa uzio kwa kutumia matofali, naomba nitumie nafasi hii kumuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri aweze kufanya tathmini kwa kuzingatia maombi aliyoyasema Mheshimiwa Charles Kajege na afahamu kwamba ni kiasi gani cha fedha zinahitajika kwa ajili ya kujenga uzio huu kwa matofali kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge, na aweze kuweka katika mipango na bajeti ya halmashauri, kwa maana ya mapato ya ndani ili hatimaye waje waweze kujenga uzio huu kwa kiwango alichokitaja Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira, nimwite sasa Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Shally Raymond kwa niaba ya Mheshimiwa Esther Malleko.

Na. 550

**Udhibiti wa Uharibifu wa Mazingira**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za kibinadamu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za kibinadamu unatokea katika sekta nyingi nchini. Ili kudhibiti uharibifu huo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuandaa sera, sheria, kanuni, mikakati na miongozo mbalimbali inayobainisha hatua zinazochukuliwa kukabiliana na changamoto hizo. Hii inajumuisha Sera ya Taifa ya Uhifadhi wa Mazingira ya mwaka 2021, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ikisomwa pamoja na Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 5 ya mwaka 2025, na Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi ya Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2022 – 2032.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu uhifadhi wa mazingira na changamoto za mabadiliko ya tabianchi kupitia njia mbalimbali, ikiwemo pamoja na vyombo vya habari, ziara za viongozi na mafunzo shuleni, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa pamoja na juhudi zote hizo za Serikali bado uharibifu ni mkubwa sana wa mazingira; je, Serikali imefanya tathmini gani kuona sasa ni wakati mwafaka kabisa kuleta ufanisi katika sheria hizo na sera ambazo ziko zimeshapangwa kama alivyoeleza kwenye jibu la msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mlima Kilimanjaro ni kivutio kikubwa sana na kinaingiza hela nyingi nchini. Mlima huo, kivutio hicho ni kwa ajili ya theluji iliyo juu ya mlima ulio chini ya *equator*. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha theluji ile haimaliziki kuyeyuka? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza Mheshimiwa Malleko, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoeleza katika jibu letu la msingi kwamba moja miongoni mwa njia ambazo tumezitumia ama tunaendelea kuhakikisha kwamba tunadhibiti athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi kama tulivyoeleza kwamba tuna sheria, tuna miongozo, tuna kanuni, na tunazo kampeni mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa, ndani ya sheria hizi, ndani ya miongozo hii, ndani ya kanuni hizi, ndani yake mna maelekezo ya kampeni mbalimbali zikiwemo kampeni za utunzani wa vyanzo vya maji, zikiwemo kampeni za upandaji wa miti, zikiwemo kampeni za matumizi ya nishati safi ya kupikia, lakini zikiwemo kampeni za utoaji wa elimu kwa wananchi, lakini zikiwemo kampeni za kuendelea kutafuta fedha ili lengo na madhumuni tuhakikishe kwamba tunapambana kwa vitendo dhidi ya athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo la athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi Serikali haijalinyamazia kimya na hatua zilichukuliwa, zinachukuliwa na zitaendelea kuchukuliwa dhidi ya athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ipo mikakati mbalimbali ambayo kama Serikali tumechukua katika kuhakikisha kwamba tunadhibiti hali ya mmomonyoko ama hali ya uyeyukaji wa theluji ama barafu katika Mlima Kilimanjaro. Sisi Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na *KINAPA* tumechukua hatua madhubuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hivi karibuni tulishiriki mkutano mkubwa wa Kimataifa, ulifanyika pale Tajikistan. Ulikuwa unazungumzia masuala ya *Glaciers' Conservation*, namna ambavyo tutahifadhi barafu na theluji kwa zile nchi ambazo zina milima yenye barafu duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine tulikubaliana kwa kauli moja, hatua ya kwanza twende tukadhibiti matumizi ama shughuli za kibinadamu zinazofanyika katika milima hiyo, lakini tulikubaliana twende tukatafute fedha, kwa sababu tunaamini haya yote yatafanyika baada ya kupata fedha ndiyo tunakwenda kuhifadhi milima yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulikubaliana kwamba tukapande miti ya kutosha, lakini tuwahimize wananchi wa nchi husika waache kuchoma moto na kufanya shughuli nyingine ambazo kwa namna moja zitapelekea uharibifu na kupungua kwa theluji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asya.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na uchafuzi wa kimazingira katika kingo za bahari na mito, na ukizingatia fukwe hizi za bahari tunazitegemea sana kwenye masuala mazima ya kuhamasisha utalii ndani ya Taifa letu, imekuwa ni sehemu ya kuleta mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kingo hizo za bahari uchafu unavyoenda baharini pia unapelekea madhara mbalimbali ndani ya bahari na kupelekea maradhi mbalimbali. Nini mkakati wa Serikali wa kuzisimamia fukwe hizi na kuzisimamia vizuri ili kuweza kuyatunza mazingira hayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Asya, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna baadhi ya shughuli zinafanyika katika kingo za bahari lakini sio tu kwenye kingo za bahari hata kwenye kingo za mito, kingo za maziwa ambazo ni sehemu muhimu ya vyanzo vya maji vinavyosaidia shughuli nyingi za kiuchumi na mambo mengine katika nchi yetu na shughuli hizi zinapelekea kuchafua baadhi ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti sasa zipo hatua ambazo kama Serikali tumezichukua; kwanza ni kusimamia sheria, hilo ndilo la kwanza, kwa sababu watu wengi wanafahamu kwamba kutupa taka maeneo hayo ama kufanya uchafuzi ni moja miongoni mwa makosa. Sasa sisi kama Serikali tumeendelea kusimamia sheria, sheria inayosimamia mazingira hasa mazingira ya pembezoni mwa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumekuwa tunaendelea kutoa elimu kupitia makongamano, kupitia washa lakini kupitia shughuli mbalimbali za kimazingira, lakini kikubwa zaidi tumeendelea kusisitiza wananchi, kwamba shughuli zinazofanyika katika maeneo haya ya fukwe zisiharibu mazingira, kwa sababu mazingira yetu ndio kitu pekee ambacho tunakitegemea, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Jonas Zeeland.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kutokana na mabadiliko ya tabianchi Mto Mbulumi umekuwa ukileta athari kubwa sana kila mwaka katika Vijiji vya Kilimanjaro, Kichangani, Dunduma na Kisala na vijiji hivi vipo kwenye hatari ya kupotea kabisa, je, nini mkakati wa Serikali katika kuudhibiti huu mto ili usiendelee kuleta atharai katika hivi vijiji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya, kwa kweli kila anaponikuta lazima aniambie

changamoto hii kiasi kwamba kuonesha kwamba wananchi imekuwa ni changamoto kubwa, lakini ni kweli kwamba tumeshakaa na Mheshimiwa Mbunge, tumeshazungumza na kuna kipindi alikuja na Madiwani wake tukakaa tukazungumza Madiwani wenye kata hizo na vijiji hivyo. *Of course* jambo hili ni jambo ambalo limewagusa wananchi wa maeneo hayo, nimwambie Mheshimiwa kwamba tayari Serikali imeshatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakwenda kujenga kuta na kushughulikia changamoto zote ambazo aidha mito ama bahari, ama maziwa maji yanaingia kwa wananchi yanakuja kuleta changamoto, lakini kubwa nimwambie Mheshimiwa kwamba kama tulivyopanga, tulivyokubaliana kabla Bunge hili halijamaliza basi tutaona namna ya kwenda na kukaa na kuzungumza na wananchi kuona namna ambavyo tunaweza kuwasaidia, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ni kinara wa utunzaji wa misitu inayovunwa hewa ya ukaa, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia hawa wananchi wa Wilaya ya Tanganyika ambao wamevuna tani za *carbon* ambazo hazina mnunuzi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kakoso kutoka Wilaya ya Tanganyika kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii niwashukuru na kuwapongeza sana Wilaya ya Tanganyika na wilaya nyingine kwa kuwa wameitikia wito wa Serikali wa kuendelea sasa kuitumi hii fursa ya kutunza misitu na kuweza kupata *carbon* ya kutosha ili tuweze kutengeneza miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ikiwemo shule, kujenga barabara, kujenga maji na kujenga hospitali za kisasa.

Mheshimiwa moja ya miongoni mwa mkakati mkubwa wa Serikali hasa baada ya kuanzishwa kwa hii biashara ya *carbon* ni kuhakikisha kwamba tunawatafutia wananchi masoko ya kutosha na ya uhakika ya *carbon* hii. Tayari Serikali imeshawakaribisha makampuni mbalimbali kuja kuwekeza pamoja na kuiweza kununua na kuweza kupata fedha za kigeni za kuweza kusaidia. Nimwambie Mheshimiwa kwamba jambo hili lipo kwenye mchakato Serikali inalifanyia kazi, wakati utakapokuwa tayari tutaona namna ambavyo Serikali inaweza kuchangamkia fursa hii na wananchi wakanufaika, ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, nimwite sasa Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, aweze kuuliza swali lake.

Na. 551

**Athari za Ufugaji Samaki kwa Njia ya Vizimba**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza: -

Je, zipi athari za kisayansi zinazosababishwa na ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa hapa nchini hakuna athari za kisayansi ambazo zimesababishwa na ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba, hii ni kwa sababu ufugaji unafanyika katika maeneo yanayokidhi vigezo vya kisheria na kitaalamu. Maeneo hayo yanabainishwa kwa utafiti na tathmini ya athari za mazingira na jamii inayofanywa na Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi

Tanzania *(TAFIRI)*. Vilevile wafugaji wa samaki kwa vizimba wanafundishwa jinsi ya kutumia mbinu bora za ufugaji wa samaki kwa vizimba ikiwa ni pamoja na matumizi ya chakula bora, vifaranga vya samaki wenye asili ya eneo husika na udhibiti wa magonjwa. Aidha, ufugaji wa samaki kwa vizimba umekuwa na mafanikio katika nchi kadhaa duniani hususani Misri, Uganda na Zambia ambapo umechangia kuongeza kwa uzalishaji samaki katika nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, iwapo ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba utafanyika bila kufuata taratibu, athari zinazoweza kujitokeza ni pamoja na uchafuzi wa mazingira na upotevu wa bioanuai za asili (*genetic pollution*). Hivyo, Wizara inaendelea kujenga uwezo wa kuwasimamia wafugaji wa samaki kwa njia ya vizimba ili kuzingatia sheria, kanuni na miongozo kwa lengo la kuwa na ufugaji wenye tija, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nishukuru kwa majibu ya Serikali, lakini katika majibu ya msingi Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza wazi kwamba ufugaji huu usipofanyika kwa kufuata kanuni unaweza kuwa na athari kwenye mazingira, lakini na upotevu wa bioanuai za asili na hili linaweza kupelekea athari na upotevu wa samaki wa asili.

Nini sasa mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba kunakuwa na ufuatiliaji na usimamizi wa karibu ili kuepusha athari hizi zinazoweza kusababisha kupoteza samaki wa asili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili; kufuatia uwekezaji wa ufugaji wa vizimba kumekuwa na changamoto ya baadhi ya wafugaji kukosa soko la samaki kwa sababu uzalishaji umekuwa mkubwa na mojawapo ni moja ya kikundi kwenye jimbo langu, Jimbo la Ukerewe, Kikundi cha Bagayo, wamevuna karibu tani 12 lakini wamekosa soko. Nini sasa mkakati wa Serikali kuwasaidia vikundi kama hivi ili iweze kuwaongezea tija? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kwamba tunalinda mazalia ya samaki asili ni pamoja na kutoruhusu vizimba kuwekwa mahala popote na ndio maana tumesema kwamba kabla ya kuweka vizimba ni lazima Serikali kupitia *TAFIRI* ijiridhishe ni eneo gani linaweza kuwekewa vizimba na eneo gani haliwezi kuwekewa vizimba, sio tu kiholela kwamba mtu anachukua vizimba anapeleka popote kwenda kuweka vizimba, hiyo hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana watu wetu, wataalamu wetu wanajua maeneo yote katika Ziwa Tanganyika, katika Ziwa Nyasa tumeshakamilisha ufuatiliaji wa kujua wapi tunaweza kuweka vizimba, Ziwa Victoria pia tunafahamu. Kwa hiyo tunapokwenda kuweka vile vizimba ni maeneo kwanza ambayo sio ya mazalia ya samaki asilia, tunakwepa mazalia asilia yaendelee kujizalia kadri inavyowezekana. Kwa hiyo, vizimba hivi vevyewe vinakwenda kuwekwa katika maeneo ambayo hakuna mazalia kabisa ya samaki asilia na ndio maana uzalishaji unaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili la kukosa soko la Samaki, nimuombe Mheshimiwa Mbunge baada ya kikao hiki tukutane tuwaunganishe wafanyabiashara wake, wafugaji wake wa Samaki na wafanyabiashara wakubwa wa samaki, kwa sababu taarifa tulizonazo ni kwamba tuna mahitaji makubwa ya Samaki kuliko uzalishaji wa samaki tulionao. Sasa nitashangaa sana samaki hawa kukosa soko wakati bado nchi inahitaji samaki pengine labda wafugaji wetu wamekosa *network* ya kujua wapi wanaweza wakauza hawa samaki. Serikali ipo tayari kumuunganisha Mheshimiwa Mbunge na wafanyabiashara wakubwa wa samaki ili tuone namna ya kuwasaidia wavuvi wetu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Waziri, mbali na kwamba Serikali mnahamasisha ufugaji wa samaki kupitia vizimba, lakini vilevile mliwahamasisha wafugaji kujiunga kwenye vikundi ili muweze kuwapatia vifaa vya kisasa waweze kuvua kisasa. Sasa unajua wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini ni wavuvi kweli kweli na wamejiunga kwenye vikundi, ni lini sasa Serikali mtawawezesha vifaa vya kisasa ikiwepo na maboti waweze kuvua kisasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kwanza nimpongeze sana dada yangu Ester Bulaya, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kufuatilia maendeleo ya watu wake na tumeshapokea orodha ya vikundi kutoka katika Jimbo la Bunda Mjini, Bunda Vijijini lakini pia Mwibara ambapo Mheshimiwa Mbunge ameleta orodha ya majina ya vikundi vyake. Tumeshatoa vizimba na boti na nyenzo za kuvulia samaki kwa vikundi mbalimbali katika eneo la Ziwa Victoria; awamu ya kwanza tulitoa vizimba vya kutosha, sasa tupo kwenye hatua ya pili ya kutoa vizimba na tumeshaanzia Geita, tupo Mwanza sasa tunakuja Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mbunge kwamba baada ya wiki moja au mbili tunakwenda kugawa vizimba vingi sana katika eneo la Bunda, Tarime kwa Esther Matiko, tutakwenda kugawa vizimba na nyenzo za kuvulia ili kuhakikisha kwamba wavuvi wetu wa samaki wanakwenda kupata uzalishaji mkubwa wa samaki katika eneo hilo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tuwatangaze wageni ambao wapo ndani ya ukumbi wetu leo ili waweze kuwapa nafasi wageni wengine, tuna wageni wengi.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni nane wa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini na hawa ni Chama cha Mabroka wa Madini Tanzania

(CHAMMATA) kutoka Mkoa wa Arusha, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna wageni wa nne wa Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, hawa ni viongozi wa *Jubilee Allianz Tanzania* na *Upland Centre* Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, huyu ni Mchungaji Emmanuel Irunde Kidua, Mchungaji Mkuu wa Kanisa la *TAG,* Kisande Chemba Mkoa wa Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, huyu ni ndugu Popat Prakash Popat, rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu Bungeni. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, huyu ni Rashid Tibita, rafiki yake kutoka Kyerwa, Mkoani Kagera. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, hawa ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa wili wa Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, hawa ni marafiki zake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa tatu wa Mheshimiwa Venant Daud Protas Mbunge, hawa ni wapiga kura wake kutoka Igalula, Mkoa wa Tabora. Siwaoni, labda hawajaingia.

Tuna wageni saba wa Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani Mbunge, hawa ni Maafisa Tarafa kutoka Tandahimba Mkoa wa Mtwara, karibuni sana, Maafisa Tarafa. *(Makofi)*

Ana wageni wengine, hapana; tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, hawa ni viongozi wa

Mamlaka ya Maji Chunya *(CHUWASA)* kutoka Mkoa wa Mbeya, karibuni sana wageni. *(Makofi)*

Wageni 25 wa Mheshima Abdallah Jafari Chaurembo, hawa ni Wenyeviti wa Mitaa kutoka Chamanzi Jimbo la Mbagala Mkoa wa Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, hawa ni viongozi wa Chama cha Walimu kutoka Masasi, Mkoa wa Mtwara, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna wageni sita wa Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, hii ni Kamati ya Utekelezaji ngazi ya Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma, wako pale karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 25 wa Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, hawa ni watumishi wa Halmashauri ya Kiteto wanajiita ni kundi la *Super Women Group* kutoka Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 84 wa Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, hawa ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Nalopa kutoka Jijini Arusha, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna wageni 14 wa Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, hawa ni Maafisa Elimu Kata kutoka Wilaya ya Tanganyika, Mkoa wa Katavi, wako pale, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; hawa ni Ndugu Abby Sanga. *(Makofi)*

Pia tuna wanafunzi 70 na viongozi watano wa Chama cha Skauti kutoka Shule za Wilaya ya Ubungo, karibuni sana *boy scouts* na *girl guides,* tunawaona pale. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 55 na walimu sita wa Shule ya Awali na Msingi Resin kutoka Kigamboni, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Maida Abdallah kutoka Geita. Wageni watatu kutoka Geita, naona hawajaingia. *(Makofi)*

Halafu tuna wageni saba wa Mheshimiwa Katani, hawa ni viongozi wa Chama, hawa nadhani nilishawasoma.

Wageni saba wa Mheshimiwa Katani, wako pale, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na maswali, twende sasa Wizara ya Viwanda na Biashara, yule aliyeteuliwa kuuliza kwa niaba ya Mwenyekiti basi apate nafasi ya kuuliza swali.

Na. 552

**Kuanzisha Viwanda vya Kuongeza Thamani ya Mazao ya Misitu**

**MHE. EDWIN E. SWALLE K.n.y. MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha eneo mahsusi la viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya misitu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, ujibu swali hilo sasa na mimi nakusikiliza. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakubaliana na dhana ya kuanzisha eneo mahsusi la viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya misitu kwa kuwa inaendana na mipango ya kuanzisha kongani ya viwanda ikiwa ni pamoja na mpango wa kuendeleza bidhaa za mbao zilizohandisiwa *(Engineering Wood Product Framework, 2021-2031)*, lengo ni kuongeza thamani ya mazao ya misitu kwa kuzalisha bidhaa za mbao handisiwa kama vile *veneer, plywood, marine board*, *blockboard* na samani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeandaa Mpango Maalum wa Kuendeleza Viwanda unaotarajiwa kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2025/2026. Kupitia mpango huo imepanga kuanzisha kongani za viwanda ngazi ya halmashauri nchini kulingana na rasilimali zinazopatikana katika halmashauri husika ikiwa ni pamoja na kongani ya viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya misitu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, maswali ya nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa wawekezaji wengi kwenye bidhaa za misitu hawana mpango wowote endelevu wa kuongeza thamani kwenye bidhaa za misitu na kwa kuwa Wizara hii ya Viwanda kazi yake ni uratibu wa viwanda hapa nchini, je, haioni haja sasa ya kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kuanzisha eneo mahsusi au *one stop centre* mkoani Njombe kwa ajili ya viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya misitu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, sisi kule mkoani Njombe ikiwemo kwenye Jimbo la Mheshimiwa Deo Mwanyika pale Njombe Mjini na Jimbo la Lupembe, wapo wawekezaji wanaovuna bidhaa za misitu, lakini wanawalipa wakulima bei kidogo sana kwenye magogo na kwenye mbao. Ni lini Serikali itaweka bei elekezi kwenye bidhaa za misitu nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu wa kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na misitu nikubaliane na ushauri wako, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine tumelibeba hili kwa ajili ya kwenda kulichakata na kuona uwezekano wa kukaa pamoja ili kuweka thamani ya mazao haya na wakulima wapate faida inayotakikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei, ni kweli kabisa kwamba bei ya mbao inawezekana haijatolewa maelekezo rasmi juu ya bei elekezi na hii inatokana na biashara yenyewe ilivyo kwa maana ya viwango vya uzalishaji na ubora wa mazao yanayotokana na hili jambo.

Mheshimiwa Swalle, tumelichukua hili jambo na Wizara itakutana na ninyi Waheshimiwa Wabunge mnaotoka kwenye eneo hili ili muweze kuyaweka vizuri masuala ambayo yanahusiana na bei ambazo kwa kweli mngependa zipewe maelekezo kutoa faida kwa wazalishaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunashukuru kwa kulichukua, lakini tunaomba mchukue kwa uzito mkubwa sana uwekezaji katika sekta hii umekuwa holela. Kwa hiyo, tunaomba sana mlichukue kwa uzito, mfanye uratibu ili wananchi waone faida ya misitu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tumepokea maelekezo yako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakuruhusu, tunakushukuru kwa majibu yako.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, swali hilo litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, kwa niaba yake.

Na. 553

**Kutekeleza Mradi wa Maji Miji 28 – Mpanda**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA K.n.y. MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa Maji wa Miji 28 utaanza kutekelezwa Wilayani Mpanda kwa kutoa maji Bwawa la Milala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji - Mheshimiwa *Engineer* Andrea Kundo kwa niaba ya Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Serikali imeanza utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Miji 28 katika Manispaa ya Mpanda, Mkoani Katavi. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa dakio *(intake)* katika Bwawa la Milala lenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 13 kwa siku, ujenzi wa miundombinu ya kutibu maji *(water treatment plant)* yenye uwezo wa kutibu maji lita milioni 12 kwa siku, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 115 sanjari na ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 2,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 40% na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2025 na kunufaisha zaidi ya wananchi wapatao 245,764 waishio katika Manispaa ya Mpanda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake yenye kuleta tumaini. Mimi nataka aji-*commit* kabisa ni lini huo mradi utakwisha Mpanda wana shida ya maji sana? Hilo swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, pamoja na juhudi kubwa anazozifanya Mheshimiwa Jenista Mhagama wa Jimbo la Peramiho kuhakikisha Kijiji cha Mdunduwalo kinapata maji. Je, ni lini sasa maji yatakamilika pale Mdunduwalo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ntara kwa swali zuri, lakini pia majibu ya Serikali ni kutokana na majibu ya msingi mradi huu utakamilika mwezi Oktoba, 2025, lakini pia kwa upande wa suala la Mradi wa Mdunduwalo nimpongeze sana

Mheshimiwa Dkt. Ntara kwa kuendelea kushirikiana na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho kwa kuhakikisha kwamba wananchi wa Mdunduwalo wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua juhudi ambazo zinafanywa na Mheshimiwa Dkt. Ntara na mradi huu tayari umeshafikia 25% na mradi huu unagharimu takribani shilingi bilioni 1.3 ambao Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alielekeza Wizara ya Maji tupeleke kutokana na maombi ya Waheshimiwa Wabunge. Nimtoe hofu, wakandarasi wako *site* na wanaendelea na kazi, naamini kabisa kwamba utakamilika kwa wakati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, wananchi wa Wilaya ya Kyerwa tuliambiwa vijiji 48 kwa zaidi ya miaka 60 ya uhuru waliahidiwa wataletewa maji vijiji 48 vikihusisha Kata za Nkwenda eneo la Lunyinya, Kimuli, Nyakatuntu, Kamuli na maeneo mengine. Una neno gani kwao ambao zaidi ya miaka 61 wanasubiri maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nimshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Anatropia kwa kazi nzuri kwa kuendelea kuwasema wananchi wa Kyerwa. Natambua kabisa kwamba lengo kuu ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na falsafa ya Mama Samia kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wakati anaingia madarakani ni vijiji takribani 6,000 na kitu ndio vilikuwa na maji na sasa kati ya vijiji 12,318 ni zaidi ya vijiji 10,650 sasa vinapata huduma ya majisafi na salama. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba maendeleo ni hatua kwa hatua na tayari tumeshafikia katika hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu na vijiji hivi 48 tutaviweka kwenye mpango ili lengo kuu ni kuhakikisha kwamba wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana ili tuone namna mzuri zaidi ya kufikisha maji kwa haraka kwa wananchi wake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, mliosimama nimewaona wote. Kwa hiyo, kaeni nitawaita mmoja mmoja. Tuanze na Mheshimiwa Joseph Kamonga. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Lipangala, Kata ya Mkongobaki kilikuwa miongoni mwa vijiji vilivyopangiwa kuchimbiwa visima vile vitano. Sasa Kijiji hiki cha Lipangala kipo juu sana kwenye mwinuko mkubwa kuliko vyanzo vya maji ambavyo viko chini sana. Kwa hiyo, suluhisho pekee ilikuwa ni kisima, sasa na pale mtambo ulienda haukufanikiwa kupata maji.

Je, nini maelekezo ya Wizara kwa wataalam ili waweze kukamilisha kisima kile wananchi wa Lipangala waweze kupata maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana namshukuru sana kaka yangu kwa kazi nzuri anayoifanya kwa wananchi wake wa Ludewa na hakika pia tunamshukuru sana kwa kuendelea kushirikiana na Wizara ya Maji kutekeleza miradi ndani ya jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa eneo la Kijiji cha Lipangala ni kweli kabisa kumekuwa na changamoto hiyo na mara nyingi tukikosa maji sehemu moja tunachohitaji ni kutafuta sehemu nyingine ambayo ina maji na tukatengeneza mtandao kufika katika eneo ambalo hatujapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais wetu ni kuhakikisha Watanzania wote haijalishi unaishi wapi lengo ni kwamba wapate huduma ya majisafi na salama. Nimtoe hofu na tunatoa maelekezo kwa wataalamu wetu watuletee taarifa na tuone nini tukakifanye pale, tutaelekeza fedha na wataenda kuhakikisha kwamba wanatatua changamoto ya pale ili wananchi wako wapate huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Mradi wa kimkakati wa Benki ya Dunia kutoka Mradi wa Solai kule Tarafa ya Nambis uliasisiwa kuanza kutekelezwa mwaka huu. Je, Serikali imefikia hatua gani katika kutekeleza mradi huu kwa sasa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Zacharia, Mbunge wa Mbulu Mjini kwa kuendelea kuwa mwakilishi anayetambua maana halisi ya uwakilishi wake wa Mbulu Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Serikali ilifanya *feasibility study* kwa mradi huo na tayari tulishakamilisha *detailed design* ambayo imetupatia *cost* ya mradi huo ambapo ni takribani shilingi bilioni 85 inahitaji, lakini mradi huo unaenda kutatua changamoto katika zaidi ya vijiji 30 vya Mbulu Mjini kwa Mheshimiwa Zacharia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuharakisha upatikanaji wa fedha hizi na tayari andiko hilo limeshakuja Wizarani na Wizara inafanya juhudi stahiki kuhakikisha kwamba mradi huo unaenda kuanza mara moja na wananchi wa vijiji hivyo takribani 30 wapate huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Noah Mollel.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kulikuwepo na miradi ya maji ambayo ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais miradi ya Oldonyosambu ambayo yenye *fluoride,* Siwandeti, Tarakwa, Kiranyi na Kimnya ambayo ilitakiwa ikamilishwe kwa ajili ya wananchi kuondoa changamoto ya maji.

Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha miradi hiyo ili kuondoa shida na kero na adha ya maji kwa wananchi hao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kama ambavyo amesema Mheshimiwa Mbunge na Serikali tunatambua hilo na *status* ya sasa namuomba Mheshimiwa Mbunge tukubaliane baada ya kutoka hapa niweze kufuatilia na niweze kumpatia majibu stahiki kwa ajili ya wananchi wake wa jimbo lake. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Masache Kasaka.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, Chunya Mjini tupo kwenye Mradi wa Miji 28 lakini mpaka sasa hivi mradi huu wa maji haujaanza na wananchi wa Chunya wanachohitaji ni maji.

Je, ni upi mpango wa Serikali wa muda mfupi kuhakikisha kwamba tunaongeza upatikanaji wa maji hasa kupitia visima virefu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na namshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Masache Kasaka, Mbunge mahiri kabisa kutoka Chunya na sisi Wizara Mheshimiwa Mbunge tumekuwa tukiwasiliana na amekuwa akisisitiza kuhusu hili na kwa maslahi ya wananchi wake

mradi wa matokeo ya haraka ambao unaendelea kutekelezwa na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2025, nikutoe hofu huu mradi unaenda kufufua visima ambavyo sasa ndio itakuwa suluhisho la muda mfupi wakati tukiwa tunasubiri Mradi wa Miji 28 utakapokamilika. Nimtoe hofu mradi huu utaenda kutatua changamoto ya muda mfupi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, Serikali ya Awamu ya Sita imeipa Wilaya ya Mwanga zawadi kubwa sana ya Mradi wa Same – Mwanga – Korogwe. Sasa swali langu ni je, ni lini mradi huu utafika katika moja ya vijiji vikubwa vya Wilaya ya Mwanga, Kijiji cha Kifaru kilometa zisizozidi mbili kutoka mradi ulipoishia? Ahsante.

**MWENYEKITI**: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na namshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Anania, Mbunge wa Mwanga. Ni kweli kabisa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliwekeza mradi mkubwa sana Same - Mwanga na tayari kwa *phase* ya kwanza umeshakamilika mpaka katika eneo la Kisangiro hapo maeneo yote yanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunafahamu kuna umbali wa kwenda katika Kijiji cha Kifaru, hiyo inakuja katika *phase* ya pili na katika *phase* ya pili kutokana na bajeti yetu ya mwaka unaokuja kuna takribani shilingi milioni 150 itahitajika kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunafikisha mradi huo katika Kijiji cha Kifaru. Nimtoe hofu, sisi tunaenda kuhakikisha kwamba utekelezaji huo unafanyika kwa haraka ili wananchi wa eneo la Kifaru wapate huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tunataja majina ya wageni kuna jina moja kidogo lilikuwa limechanganyika.

Tuna mgeni ambaye anaitwa Fadhili Sanga ambaye ni kaka yake na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Festo Richard Sanga kutoka Makete, Kijiji cha Bulongwa, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunaendelea Wizara ya Kilimo, nimwite sasa Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kwa niaba yake Mheshimiwa Fatma Toufiq.

Na. 554

**Ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji – Kalambo**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ K.n.y. MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa skimu za umwagiliaji utaanza na kukamilika katika maeneo yote ya Wilaya ya Kalambo yaliyobainishwa kuwa na fursa za kilimo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri, Mheshimiwa David Silinde.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, katika mwaka 2024/2025 Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini ikiwemo upembuzi yakinifu na usanifu wa Skimu za Ilimba, Mkowe, Santamaria, Sopa, Kamawe, Kasanga, Katete, Mtuntumbe, Kasitu, Tatanda, Mao, Katazi, Mnazi, Kaluko, Kilesha, Kambo, Kalembe, Ulumi na Katuka zenye ukubwa wa jumla ya hekta 21,300 zilizopo katika Wilaya ya Kalambo. Upembuzi wa skimu hizo unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026 na kuanza taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi. Aidha, mradi wa Skimu ya Selengoma yenye ukubwa wa hekta 1,500 iliyopo katika Wilaya

ya Kalambo upo katika hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, skimu ya umwagiliaji iliyopo Kijiji cha Ulumi, Kata Ulumi ujenzi wake haujakamilika; je, ni lini ujenzi wa skimu hii utakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, lini Skimu ya Umwagiliaji ya Taqwa iliyopo katika Wilaya ya Chemba itaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Skimu ya Ulumi ilijengwa zamani bila kufuata zile taratibu za mkandarasi na sisi sasa hivi kupitia Tume ndio maana tunafanya usanifu upya ili tuanze kuijenga upya iweze kuendana na wakati na isiwe inaharibika kila wakati. Kwa hiyo, ndio kazi kubwa ambayo tunaifanya sasa hivi na tukimaliza tunaweka mkandarasi ambaye ataanza kuijenga upya kama ambavyo mchoro utakavyokuwa umeainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya Taqwa na yenyewe ni moja ya skimu ambazo zipo katika utekelezaji na nimthibitishie tu kwamba katika hatua tulizopo sasa za kutafuta mkandarasi akishakuwa amepatikana basi ujenzi wake utaanza mara moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kalenga lina skimu zaidi ya 19 ambazo ni chakavu sana. Nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba skimu hizi zinakarabatiwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri, kwa niaba ya Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimuondoe shaka Mheshimiwa Tendega kwamba katika Jimbo la Kalenga hizo skimu zote 19 na zenyewe zinafanyiwa usanifu wa kina na upembuzi yakinifu na tukishakamilisha maana yake zitaanza kujengwa zote. Hayo ni maelekezo ambayo tulipewa na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge zitafanyiwa kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Selemani Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Skimu ya Umwagiliaji ya Lyamalagwa, Kata ya Sigili, Jimbo la Bukene ni skimu kubwa sana ambayo itakapokamilika itagharimu karibu shilingi bilioni 29 na wananchi wanaisubiri kwa hamu kubwa sana, lakini mkandarasi amekuwa na *speed* ndogo sana.

Je, Serikali ina kauli gani kuhusu kumharakisha huyu mkandarasi ili aweze kukamilisha Skimu hii ya Lyamalagwa, Sigili ili wananchi waanze kunufaika na kilimo cha mpunga? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimuondoe hofu Mheshimiwa Selemani Zedi wa Jimbo la Bukene kwamba skimu hiyo tayari ina mkandarasi ambaye yuko kazini, lakini bahati mbaya ni kwamba yuko *slow* na ninailekeza Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwenda katika eneo hilo kumsukuma huyu mkandarasi, lakini kuhakikisha kuona ni changamoto gani inamfanya achelewe kufanya hiyo kazi. Kwa hiyo, haya ni maelekezo na ninayatoa hapa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, niliwaona tutakwenda kwa Mheshimiwa Innocent Kalogeris, Mheshimiwa Mtaturu, halafu Mheshimiwa Fiyao. Tunaanza na Mheshimiwa Kalogeris.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Skimu ya Umwagiliaji ya Lubasazi iliyopo Kata ya Kolero zaidi ya shilingi milioni 800 zimetumika na huu ni mwaka karibu wa nane hakuna mwendelezo wake. Nini kauli ya Serikali ili wananchi wapate kutumia ile skimu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kabla skimu nyingi ambazo zilikuwa zinajengwa hapa nchini zilikuwa hazikufanyiwa tunasema usanifu wa kina na upembuzi yakinifu, matokeo yake skimu nyingi zilikuwa zinapelekwa fedha bila kujua ukubwa wa kazi ya eneo husika.

Kwa hiyo, sisi sasa hivi tunachokifanya ni kurudia na kujua ukubwa wa kazi ili tupate gharama halisi, tupate mkandarasi ambaye atazijenga skimu hizo kwa ufanisi mkubwa. Kwa hiyo, miongoni mwa skimu ambazo tunakwenda kuzifanyia marejeo ni pamoja na hii skimu ambayo ameieleza Mheshimiwa Kalogeris ya Malachanjo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jumanne Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Skimu ya Umwagiliaji ya Mang'onyi ni skimu ambayo ilishatengewa zaidi ya shilingi milioni 700 na Serikali na tulikuwa tunamsubiri mkandarasi ili apatikane aanze ujenzi. Nimefika Wizarani mara mbili na Waziri unajua, niliambiwa iko kwenye hatua ya kwenda kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata mkataba.

Nini hatua iliyofikiwa ili wananchi wa Mang'onyi waweze kupata skimu wanayoisubiri? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Mheshimiwa Mtaturu waambie wananchi wako kwamba tayari skimu hii tumeshapata barua kutoka kwa Mwanasheria Mkuu kwamba sasa tuanze, tumekubaliwa kwa ajili ya utekelezaji. Kwa hiyo, jambo hili lipo katika hatua tusema ya mwisho kabisa na tutaanza utekelezaji hivi karibuni. Ahsante. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Stella Fiyao.

**MHE. STELLA F. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, nataka kujua ni lini Serikali mtakamilisha *scheme* ya umwagiliaji katika Kata ya Chitete ndani ya Wilaya ya Ileje hasa ukizingatia kwamba skimu hii ikikamilika itahudumia wananchi wa wilaya mbili kwa maana ya Mbozi, Kata ya Nyimbili na Ileje, Kata ya Chitete, ni lini mtakamilisha ili iweze kuwanufaisha wananchi wetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba skimu ile inafanyiwa upembuzi yakinifu na tupo katika hatua za mwisho na tukishamaliza tutaanza ujenzi na tunatambua ukubwa wa ile Skimu ya Chitete iliyopo katika Wilaya ya Ileje, kwa hiyo tuwaeleze wananchi kwamba Serikali ipo katika hatua za mwisho kabla ya kuanza ujenzi wa skimu hiyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Elibariki Kingu, kama nilikuona.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nilikuwa naomba Serikali itupe majibu, ilitupa ahadi kutujengea skimu ya umwagiliaji katika Kata ya Mhungira, Iyumbu lakini mpaka leo tunapozungumza jambo hili ni kama vile limepotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali itupe majibu Wana-Ikungi Magharibi, je, skimu hii bado wana mpango wa kuijenga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimwondoe shaka kaka yangu Mheshimiwa Kingu, wathibitishie tu wananchi kwamba ahadi ya Serikali ipo pale pale, tupo katika hatua za kutafuta fedha ili tuanze ujenzi na wewe kwa sababu ni moja ya Wabunge mahiri, tutahakikisha skimu hiyo inajengwa kwa faida ya wananchi wako na Tanzania nzima kwa ujumla, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Afya, nimwite sasa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda aweze kuuliza swali lake.

Na. 555

**_MSD_ Kutopeleka Majokofu ya Mochwari Kituo cha Afya – Mugeta - Bunda**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza: -

Je, kwa nini tangu mwaka 2018 hadi leo *MSD* haijapeleka majokofu manne ya mochwari katika Kituo cha Afya Mugeta – Bunda?

**MWENYEKITI:** Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Godwin Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 21 Februari, 2024 Serikali kupitia Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* ilipeleka jokofu lenye uwezo wa

kuhifadhi miili sita katika Kituo cha Afya Mugeta na hadi sasa jokofu hili linafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kununua na kusambaza vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa wakati Kituo cha Mugeta kinajengwa tulipewa mwongozo kwamba kituo kile kinajengwa kwa shilingi milioni 700; shilingi milioni 400 ya ujenzi na shilingi milioni 300 ya vifaa, na shilingi milioni 300 hiyo iende *MSD* sio kwamba ni hela ya kukopa wala ya kuomba, na mpaka sasa tumepokea vifaa vya shilingi milioni 161, vifaa tiba vya Kituo cha Mugeta, lakini bado shilingi milioni 139 ambazo tuliambiwa tunapewa *x-ray* na sasa ni lini hiyo *x-ray* ya Mugeta itaenda kwa shilingi milioni 139 iliyobaki *MSD?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali ina mkakati gani sasa wa kumaliza Hospital ya Wilaya ya Butiama ya Bunda?

**MWENYEKITI:** Hebu, kisemeo chako kimezima.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza Hospitali ya Wilaya ya Bunda ya Mkama, mkakati gani wa Serikali wa kumaliza hiyo hospitali kwa sababu bado hali yake siyo nzuri?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kwa kweli amekuwa ni mpambanaji na wakati wote akizunguka Wizarani kuhakikisha fedha zinakwenda kwenye wilaya yake hiyo ya Bunda.

Kwanza nimwambie kwamba amesema kuna zaidi ya shilingi milioni 130 ambazo bado zipo *MSD* kwa ajili ya *x-ray* na nimwambie tu kwa sababu pale kwenye kile kituo kuna utaratibu sasa wa kutaka kujenga hilo jengo la *x-ray,* kwa hiyo jengo la *x-ray* likiisha basi na hizo fedha zitatumika kwa ajili ya kuleta *x-ray* ambayo inatakiwa kwenye eneo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali lake la pili kuhusu hospitali yake ya wilaya anajua yeye mwenyewe alifuatilia na mwezi wa 12 ziliingia shilingi milioni 980 na zimefanya kazi kumalizia yale majengo yaliyokuwepo na siyo muda mrefu halmashauri yake iliandikiwa wakapewa *ceiling* ya shilingi milioni 500 na wameshaainisha vipaumbele vyao na sio muda mrefu shilingi milioni 500 hiyo itaingia ili kuweza kumalizia majengo yaliyopo pale kwenye hospitali yake.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kuwa utaratibu uliopo hivi sasa wa kupeleka dawa katika halmashauri zetu kutoka *MSD* unategemea fedha ambazo zinatoka halmashauri ili kuagiza hizo dawa; je, Serikali haioni sasa wakati umefika wa kuipatia mtaji wa kutosha *MSD* ili iweze kwenda na wakati katika kuagiza dawa na kupeleka dawa katika halmashauri zetu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu tu swali zuri la Mheshimiwa Mbunge, ni kweli kwamba tunatenga hapa shilingi milioni 200 ambazo ndiyo hizo zinakwenda kwenye halmashauri zetu na ndiyo zinazotumika kupeleka dawa, kununua dawa sasa kupeleka kwenye halmashauri zetu, lakini

anazungumzia jambo la *MSD* kupata mtaji na mnajua hapa tayari *MSD* ilishapewa shilingi bilioni 100 kwa ajili ya mtaji na Serikali itaendelea kufanya hivyo na kuna namna ambavyo Serikali inafanya ili pia *MSD* iweze kukopa na kushirikiana na wadau mbalimbali kuweza kufikia hilo lengo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, nilikuona.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Chuo cha Afya *PSI* kilichopo Iringa kimechakaa sana na majengo yaliyoanza kujengwa hayajamaliziwa, je, mna mpango gani wa kumalizia chuo kile?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa zaidi ya shilingi bilioni 187 kwa ajili ya ujenzi wa vituo mbalimbali kwenye hospitali zetu za mikoa, lakini pamoja na ukarabati wa vyuo vya kufundishia wataalam wetu, lakini pia kujenga vyuo vipya, nimwombe Mheshimiwa Mbunge tukimaliza hapa, tukae chini tuangalie katika hicho chuo chake, katika fedha kama chuo chake kimepangiwa ili niweze kumpa jibu halali kwamba kimepelekewa shilingi ngapi ili hapa nisije nikataja *figure* ambayo siyo sahihi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Hospitali ya Manyamanyama, Kituo cha Afya cha Manyamanyama, mwanzoni ilikuwa iwe Hospitali ya Wilaya ya Bunda kutokana na idadi kubwa ya huduma inayotoa mpaka kwenye wilaya za jirani kule.

Je, Serikali hamuoni kwamba kuna haja ya kuiongezea mgao wa vifaa tiba ili iweze kutoa huduma stahiki maana sasa hivi imeelemewa ukilinganisha na huduma inayoitoa, inapata vifaa tiba kidogo na dawa, lakini huduma inayoitoa ni kubwa mpaka kwenye wilaya za jirani?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu alichokiuliza Mheshimiwa Ester Bulaya kipo *straight forward* na ukweli ni kwamba inatakiwa upeleke dawa kulingana na mahitaji, lakini kulingana na idadi ya watu na huduma kituo chenyewe kinavyotoa.

Kwa hiyo nimuombe sasa tukija hapa tuwasiliane na Mganga Mkuu wa Wilaya halafu sasa atuletee idadi halafu tuanze *process* ya kuiongezea dawa na vitu vingine kwenye kituo hicho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, nimwite sasa Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi aweze kuuliza swali lake na kwa niaba yake litaulizwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

Na. 556

**Ujenzi wa Mitaro katika Barabara ya Lupiro – Namtumbo**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali isijenge mitaro katika Barabara ya Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Namtumbo ili kuinusuru isiendelee kuharibiwa na mvua?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri Mheshimiwa Godfrey Kasekenya.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesaini mkataba wa ujenzi wa Barabara ya Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo -

Lumecha (kilometa 284.5), sehemu ya Ifakara – Lupiro – Mtimbira (kilometa 112) kwa utaratibu wa sanifu na jenga *(design and build)*. Ujenzi wa barabara hii utaenda pamoja na ujenzi wa mitaro kulingana na usanifu ulivyoelekeza. Kwa sehemu iliyobaki ya barabara hii, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* itaendelea kuijenga mitaro kwa sehemu zenye uhitaji ili kuilinda barabara isiharibiwe na maji ya mvua, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, kwanza niipongeze Serikali kwa majibu mazuri ambayo yanakusudia kwenda kuijenga barabara hii ambayo inaunganisha takrabani wilaya na mikoa miwili tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili, swali la kwanza, wakati huu ambapo mkandarasi ameingia mkataba kwa ajili ya kuijenga, barabara hii imeharibika kwa kipindi hiki cha mvua, ni yapi maelekezo ya Serikali kuhakikisha barabara hii inaweza kupitika kwa kipindi hiki wakati wananchi wanaendelea kusubiri utekelezaji na ujenzi wa kiwango cha lami? Ndivyo ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameniagiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kwa ajili ya wananchi wa Makete, Mheshimiwa Waziri unaijua Barabara ya Makete Mbeya ni barabara ambayo mvua inanyesha kwa muda mrefu na wewe umekuwa ukikiri hapa mara kwa mara kwamba barabara hii inasumbua kwenye ujenzi wake. Ninavyozungumza sasa hivi mvua imesimama, hainyeshi tena, kiangazi kimeanza, lakini mkandarasi hajarekebisha barabara hii ili wananchi wangu waweze kupita katika mazingira salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba maelekezo ya Serikali muda huu, dakika hii, kwa mkandarasi yule ili barabara iweze kupitika na wananchi waendelee kufanya shughuli za kiuchumi kwenye Jimbo la Makete, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Barabara ya Ifakara – Lupilo – Malinyi hadi Lumecha ilipata changamoto kubwa ya kuharibika na kimsingi ilikuwa haipitiki kabisa, lakini maeneo mengi ambayo yalikuwa hayapitiki ni yale yenye mito na sasa hivi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna mto unaitwa Namhanga ambao ulikuwa umekata kabisa mawasiliano kati ya Malinyi na upande mwingine, tuna mipango miwili pale na hasa kwa wananchi wa Malinyi tuna mipango mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza ilikuwa ni kupeleka daraja la muda la chuma ambalo tayari tumeshaliweka na magari yenye uzito usiozidi tani kumi yanaendelea kupita, lakini mpango wa muda wa kati ni kujenga *drift* ili tuweze kuruhusu sasa magari yote yaweze kupita, lakini mpango wa kudumu ni kwamba tunaanza kujenga lile daraja kwa sababu lipo kwenye mpango wa kulijenga daraja lote ambalo tutasaidiana na wenzetu wa *World Bank* kupitia *CRW* hizo hela na tayari mkandarasi tumeshampata, kwa hiyo, tutahakikisha kwamba hiyo changamoto inaisha wakati huo mkandarasi atakayeanza kujenga kipande hicho cha kilometa 112 akiwa anafanya *mobilization*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara hii ya Makete – Mbeya, nimwagize tu Meneja wa Mkoa wa Njombe ahakikishe kwamba wakandarasi hawa wanarudi *site*, lakini kabla ya kurudi *site* warekebishe maeneo yote ambayo yalikuwa yamekatika ndipo aanze kufanya kazi sasa ya ujenzi kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Daraja la Mangara limesimama ujenzi wake sasa hivi ni takribani kama miaka miwili hivi na sababu ni kwamba mkandarasi hajalipwa *certificate* zake, nimekuja mara kadhaa

kwenye Wizara ya Ujenzi kwa ajili ya ku-*push* jambo hili na hata Mheshimiwa Naibu Waziri analifahamu vizuri, je, anataka kuzungumzia nini kuhusiana na daraja hili, sehemu ambapo takribani shilingi bilioni tano zimeingia, je, zinapotea bure tu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hizo fedha haziwezi kupotea na Serikali itahakikisha kwamba inalikamilisha hilo daraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kwamba tu hilo daraja ni muhimu kwa ajili ya wananchi na wanaolima korosho lakini pia ni daraja muhimu sana kwa shughuli za ulinzi kwa sababu ndiyo barabara ambayo tunasema barabara ya ulinzi kwa mikoa ya Mtwara na Ruvuma. Kwa hiyo tutahakikisha Mheshimiwa Mbunge baada ya mvua kukatika wakandarasi hao watarudi *site* ili kulikamilisha hilo daraja, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Bunge lilielekeza Mfuko wa Barabara kukusanya kutokana na tozo ya mafuta shilingi bilioni 850, mpaka mwezi Februari mwaka huu zimekusanywa shilingi bilioni 819; mpaka sasa hivi *TANROADS* wamepewa shilingi milioni 123 tu; lakini vilevile mnadaiwa na wakandarasi shilingi trilioni 1.3. Sasa kwa nini unawapa Wabunge majibu ambayo unajua hayatekelezeki kwa sababu hamna pesa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni kwamba nimuombe ili apate maelezo ya kina, nitamuomba afanye mambo mawili, ama atuletee swali lake la msingi ambalo litalingana na swali na

tumpe maelezo sahihi, ama tuweze kuonana baada ya hapa maana swali la msingi hapa ni kujenga mitaro kwenye barabara kwa hiyo hili swali nadhani tumuombe atuletee swali la msingi tumjibu vizuri, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema sawa lina takwimu hilo swali, kwa hiyo, kwa vile lina takwimu ni vizuri ukalileta kama swali liweze kujibiwa. Mheshimiwa Shamsia.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Ni lini Serikali itafanya ukarabati mkubwa Barabara yetu ya Kusini ya Somanga – Kibiti - Lindi kutokana na uharibifu mkubwa uliopo hivi sasa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, barabara hii ni barabara kuu ambayo inaenda Mikoa ya Kusini, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa ukienda kazi iliyokuwa inafanyika ni kujenga maeneo yote yaliyokuwa yameharibika na hasa ya madaraja, na tunachowekea sasa hivi ukienda utaona tayari tunasema tumeshakamilisha kazi ya chini na vyuma vimeanza kusimama. Maeneo yote yaliyokuwa yamechoka sasa hivi madaraja yale yanajengwa, lakini tuna mpango wa kuhakikisha kwamba tunakarabati maeneo yote yaliyokuwa yameharibika ambayo yalikuwa hayapitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mpango upo na tumekuwa tunayaongezea mara kwa mara wakati tunatafuta fedha, chanzo kikubwa na ambacho kitakuwa cha uhakika kuikarabati barabara yote ya kusini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Kuna swali lingine lipo

pale, nimwite sasa Mheshimiwa Stephen Byabato, Mbunge wa Bukoba Mjini aweze kuuliza swali lake.

Na. 557

**Kuwatambua Wakandarasi Wazawa Wanaofanya Kazi Nzuri**

**MHE. STEPHEN L. BYABATO** aliuliza: -

Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuwatambua wakandarasi wazawa wanaofanya kazi nzuri ili kuwapa motisha?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** Alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Makandarasi *(CRB)* huwatambua makandarasi wanaofanya kazi nzuri kwa kuwapatia tuzo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na tuzo za ukuaji haraka kwa wale wanaoonesha ukuaji mzuri tangu usajili, tuzo kwa wakandarasi wanaozingatia usalama kazini na tuzo kwa ajili ya kumpuni zinazomilikiwa na wanawake zenye mafanikio katika miradi. Aidha, mkandarasi anapokamilisha kazi aliyopewa vizuri kulingana na mkataba mwajiri hutoa hati maalum ya kukamilisha kazi *(Final Completion Certificate)* ambayo hutambua kuwa kakamilisha kazi yake vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stephen Byabato, swali la nyongeza.

**MHE. STEPHEN L. BYABATO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninalo swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bukoba Mjini tulipata pesa takribani shilingi bilioni 12.5 kwa ajili ya ujenzi wa njia nne kutoka katikati ya mji kwenda pembeni. Sasa napenda kufahamu, ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha inamuwezesha mkandarasi mzuri anayefanya kazi hiyo mzawa anayeitwa *Abemulo Contractors* kukamilisha kazi hiyo vizuri na kwa wakati ili na yeye tuweze kumpa pongezi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge Serikali itahakikisha kwamba kazi hiyo inakamilika ya kujenga njia nne na tuna kazi mbili pale, tuna miradi miwili, lakini mkandarasi ni huyo huyo. Kuna Mradi wa …. na huo mradi ambao unatekelezwa kwa fedha ya Serikali 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichokifanya sasa hivi, tumeshapeleka hati za madai kwa wenzetu wa Hazina ili aweze kuongeza kasi maana amerudi nyuma, aweze kuongeza kasi na kukamilisha kazi kwa sababu sasa hivi tupo kwenye 40%. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Bukoba, Serikali tutahakikisha kwamba hiyo hazi inakamilika, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea swali linalofuata. Mheshimiwa na wewe una swali? Endelea.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naomba kujua ni lini sasa ujenzi wa Barabara ya Igauli – Ilongero kilometa kumi na moja na nusu zitaanza ujenzi wake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, hii barabara iko kwenye majadiliano, tulishaitangaza, wakandarasi wameshapatikana, tuko kwenye majadiliano ya gharama za kuanza ujenzi kipande hicho cha Singida – Ilongero kilometa 11.5, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea na maswali, bado tuko katika Wizara ya Ujenzi. Nimwite sasa Mheshimiwa Aysharose Ngogholi Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake na

kwa niaba yake swali litaulizwa na Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila.

Na. 558

**Ujenzi wa Barabara ya Sepuka – Ndago - Kizaga**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA K.n.y. MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa kiwango cha lami Barabara ya Sepuka - Ndago hadi Kizaga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Barabara ya Sepuka – Ndago ni sehemu ya Barabara ya Sepuka - Ndago - Kizaga yenye urefu wa kilometa 77.4. Serikali tayari imeanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Sepuka – Ndago – Kizaga kilometa 77.4 na hadi tarehe 30 Mei, 2025 kazi za ujenzi zilikuwa zimefikia asilimia tatu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana, wanawathibitishia vipi wananchi hawa kwamba barabara hii itaisha haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, nilitaka kufahamu Barabara ya Mbalizi – Songwe – Mkwajuni, inaanza lini rasmi? Maana mlituambia mtatenga bajeti, hatujaona kinachoendelea *site*? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, barabara hii itaisha

haraka kwa sababu tayari wakandarasi wako *site* na wameshalipwa *advance* na ndiyo maana wako wameanza kufanya kazi. Kwa hiyo, cha msingi tutawasimamia ili waweze kukamilisha kwa mujibu wa mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mbalizi – Songwe, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuko tayari muda wowote kusaini hii barabara kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami kama tulivyoahidi na bado tumeipangia tena kwenye bajeti ya mwaka unaokuja ili kuendelea na ujenzi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Ni lini Serikali itajenga Barabara ya *Old Moshi* kupitia Kikarara – Kidia mpaka Kirua ambayo ina kilometa 17 lakini Serikali imejenga kilometa 4.5 tu na barabara hii ni muhimu kwa sababu inaamua hatma ya uchumi wa kata zaidi ya tano. Ni lini Serikali itamaliza barabara hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara hiyo ni muhimu na tutahakikisha kwamba tunashirikiana na wenzetu wa *TARURA* kuweza kuzijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba barabara zetu ni zile ambazo hasa zinaunganisha wilaya na wilaya, wilaya na mkoa na baadhi ambazo zinapita kwenye kata. Kwa hiyo, nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge Serikali tutahakikisha kwamba tunakamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami kwa hizo barabara alizozitaja, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri, ni lini mkandarasi atarejea katika *site* ambapo alikuwa ameshaweka vifaa vyake lakini mwaka jana mwezi wa kumi akaviondoa na watu sasa wanasubiri barabara na mkandarasi hayupo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ningeomba anitajie hiyo barabara. Maana ninajua ana barabara mbili pale. Sasa sijajua ni ipi hasa.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni barabara kutoka *airport* kwenda Kayenze ambayo inajengwa kwa kilometa 10 kutoka *airport* mpaka Kabangaja kwa awamu ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayofanya kuhusu wananchi wa Ilemela. Nataka nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mwanza, Serikali inachukulia barabara hii kama ni moja ya barabara ambayo ni *bypass* kwa watu wa kutoka *airport* wanaokwenda Mikoa ya Simiyu, Mara na Kenya. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mkandarasi huyu tumeshapokea hati zake za madai ya fedha za awali ili aweze kurudi *site* na kuanza kazi na akamilishe hizo kilometa 10, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wabunge kutoka Mikoa ya Tabora, Mbeya, Singida na Songwe, wangependa kusikia kauli ya Serikali kuhusu ukamilishaji wa barabara namba nane nchini *(trunk road* namba nane) ambayo kipande kutoka Ipole – Rungwa, Rungwa –

Makongolosi na Rungwa – Itigi hadi Mkiwa, vitakamilika lini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Kakunda na kwa niaba ya Wabunge aliowataja wa mikoa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakiri kwamba hiyo barabara aliyoitaja sasa hivi ndiyo barabara iliyobaki, barabara ndefu na barabara kuu ya nchi *ET8* na tulichopewa maelekezo ni kuhakikisha kwamba tunatafuta chanzo kikubwa cha fedha na tuko tayari tunaongea na taasisi mbalimbali za kifedha ambazo ziko tayari kuweza kuingia nazo ubia ili tuweze kujenga hiyo Barabara ya Ipole – Rungwa, lakini Mkiwa – Rungwa halafu Rungwa – Makongolosi. Kwa hiyo, tunajua itasaidia sana kuunganisha mikoa ya nyanda za juu Kusini, mikoa ya kati lakini na mikoa ya Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inaichukulia kwa umuhimu mkubwa sana hiyo barabara, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Ally Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, barabara ya kutoka Masaninga – Nangurukuru mpaka Kilwa Masoko imeharibika vibaya sana kutokana na aidha mvua, lakini pia magari mazito yanayobeba uzito mkubwa ambayo yanapeleka *materials* kwenye ujenzi wa bandari kule Kilwa Masoko. Serikali iliahidi hapa kutenga fedha kwa ajili ya kuikarabati ama kuijenga upya barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kutengeneza Barabara ya Masaninga – Nangurukuru – Kilwa Masoko?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kutokana na mabadiliko makubwa ya kiuchumi ni kweli kuna barabara ambazo zilikuwa zimejengwa kulingana na uzito ama aina ya magari yanayopita. Sasa hivi tulichofanya ni kuisanifu hiyo barabara kulingana na ukweli kwamba sasa inabeba ama inapitisha magari yenye uzito mkubwa ili sasa tuweze kuijenga kulingana na mahitaji ya sasa. Kwa hiyo, Serikali inalifahamu na tunalifanyia kazi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, nimwite sasa Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, aulize swali lake.

Na. 559

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi na Nyumba za Watumishi – Nanyumbu**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Nanyumbu pamoja na nyumba za watumishi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Daniel Sillo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu imetoa eneo Kitalu F, kiwanja namba moja kilichopo Mtaa wa Mangaka chenye ukubwa wa mita za mraba 68,682 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Nanyumbu pamoja na nyumba za makazi ya askari. Serikali inatarajia kujenga Kituo kipya cha Polisi cha Daraja B, kitakachogharimu kiasi cha fedha shilingi 802,926,788. Fedha kwa ajili ya ujenzi zitatengwa kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2026/2027. Baada

ya ujenzi kukamilika, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi ya kuishi askari polisi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, kwanza, naipongeza Serikali kwa majibu mazuri ambayo yanatia matumaini, lakini pili, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwanza kwa kutekeleza ahadi yake ya kutupatia gari kwenye kituo changu cha polisi pale Nanyumbu, kwenye Mji wetu wa Mangaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gari lile ni muhimu sana hasa ukizingatia kwamba sisi watu wa mipakani tunahitaji gari la uhakika kwa shughuli za ulinzi. Nawapongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, majibu ya Serikali yanaeleza kwamba kituo hiki cha Polisi kitajengwa kwenye Kitalu F ambapo Halmashauri yetu ya Wilaya ya Nanyumbu imetoa. Hivyo nampongeza sana Mkurugenzi kwa kutoa ardhi hii kwa ajili ya ujenzi huu. Sasa naiomba Serikali inipe *commitment,* ujenzi huu wa kituo hiki cha polisi Daraja la B, kweli utaanza katika mwaka huo wa fedha ulioutaja?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza, nipokee pongezi alizotoa Mheshimiwa Mbunge. Pongezi ziende kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutenga fedha kwa ajili ya kazi kubwa ya upatikanaji wa magari kwa ma-*OCD* wote nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikijenga Vituo vya Polisi vya makamanda wa mikoa na wilaya na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wilaya ya Nanyumbu tunajua iko mpakani na kwa ajili ya usalama wa wananchi wake, nimhakikishie Serikali imeji-*commit* kwa mwaka wa fedha

2026/2027 tunajenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Nanyumbu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kalogeris naona kama ulishauliza swali, ngoja twende kwanza huku. Waheshimiwa, tumeshawaona wote mliosimama. Kwa hiyo, naomba tu mkae. Tuanze na Mheshimiwa Esther Matiko. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nimekuwa nikifuatilia kuhusiana na ujenzi wa vituo vya kisasa na vyenye hadhi katika Wilaya za Kipolisi za Kanda Maalum Tarime – Rorya ambazo ni Sirari, Shirati, Nyamwaga, Utegi na Tarime na tunashukuru Tarime mmeanza kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa mtajenga vituo hivi vingine vya kipolisi vya hizi wilaya ambazo nimezitaja zilizoko katika Kanda Maalum ya Tarime – Rorya ikiwepo na Bunda? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana,n naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Esther Matiko amekuwa mdau sana wa Wizara ya Mambo ya Ndani, amekuwa akifuatilia ujenzi wa vituo hivi na kama ambavyo tumshajenga Kituo hiki cha Tarime – Rorya, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, vituo hivi vingine alivyovitaja pia tutaviweka kwenye mpango. Hatutajenga mara moja, tutajenga awamu kwa awamu. Serikali inatenga fedha kila mwaka wa fedha. Kwa hiyo, nimhakikishie hivyo alivyovitaja pia tutaweka kwenye mpango tayari kwa kutengewa fedha kwa ajili ya kujengwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru, nyumba za askari wetu wa Tabora Mjini zimechakaa

na hazifanani kabisa na watu kuishi ndani ya nyumba zile. Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba mpya katika eneo hilo hilo ili askari wetu waweze kuishi kwenye mazingira salama na rafiki kutokana na kazi ambayo wanaifanya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Mwaifunga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Polisi itafanya tathmini kuona je, kama hizo nyumba zinafaa kwa ukarabati au kujenga upya na baada ya tathmini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba nyumba hizo tunazijenga vizuri ili askari wetu waweze kukaa katika mazingira bora na kufanya kazi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa wala msisimame, tumeshawaona. Kwa hiyo, tutawataja tu mmoja mmoja. Mheshimiwa Asha Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kuwa vituo vya polisi na makazi ya polisi ni muhimu sana katika kila maeneo, sasa je, ni lini Serikali itakuja na mpango mkakati wa kuainisha vituo vya polisi na makazi ya polisi nchi nzima badala ya kila mtu kuomba kwenye jimbo lake kama hivi ilivyo sasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asha Juma kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Wizara ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ina mpango wa kujenga vituo vya polisi

kwenye kata zote kwa upande wa Tanzania Bara na shehia kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba pia na baada ya ujenzi wa vituo hivyo vya polisi, tutatenga fedha pia kwa ajili ya ujenzi sasa wa nyumba za kuishi askari wetu katika maeneo hayo ili watoe huduma kwa wananchi wetu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona, kwanza, nianze kw akulipongeza Jeshi la Polisi nchini, juzi nilikuwa jimboni Mheshimiwa Naibu Waziri, yakatokea ya kutokea majambazi yakaingia kwenye Mji wa Mbogwe na wakakabiliana nayo na wakamaliza vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto walizonazo Mbogwe, askari hawana nyumba za kuishi, lakini pia kituo hawana. Mimi nilishachukua tayari eneo la kujenga kituo cha polisi.

Sasa swali langu la msingi, ni lini Mheshimiwa Waziri utatoa pesa ili kusudi Wilaya ya Mbogwe kituo kijengwe, lakini pia na gari wapate ili waendelee kukabiliana na majambazi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nicodemas Maganga, Mbunge wa Mbogwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tunalipongeza jeshi letu kwa kweli kwa kazi kubwa linayofanya ya kulinda raia na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameshatenga kwa halmashauri hiyo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha polisi kwa maana eneo la Mbogwe. Nimhakikishe tutaliingiza kwenye mpango ili tutengee fedha sasa upande wa Serikali ili tuweze kujenga kituo hicho cha polisi ambacho kitasaidia

usalama wa raia na mali zao katika eneo la Mbogwe, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Omar Issa Kombo.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba uniruhusu nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Mheshimiwa Bashungwa pamoja na Mheshimiwa Sillo kwa kusikia kilio cha wananchi wa Wilaya ya Micheweni kuhusu ujenzi wa Kituo kipya cha Wilaya ya Micheweni. Hivi ninavyokwambia tayari ujenzi umeanza.

Sasa naomba niulize, ni lini Serikali itawajengea polisi wetu wa Wilaya ya Micheweni makazi ya kudumu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Omar Kombo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Micheweni, sasa Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha sasa tunajenga nyumba za askari wetu katika eneo hilo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, mwaka 2021 tulianza ujenzi wa kituo cha polisi pale Kishapu na kwa bahati nzuri tumefikia hatua nzuri, shilingi milioni 100 zimetumika katika hatua ya upauaji ambayo tumeifikia kwa sasa. Hii ni nguvu za wananchi, Mfuko wa Jimbo pamoja na Mgodi wa Mwadui ambao umechangia fedha kwa ajili ya ujenzi huu. Sasa Serikali iliweka kwenye mpango wa mwaka huu ambao tunaumalizia kwamba ingetekeleza kwa ku-*support* hizi nguvu zote kwa ajili ya kukamilisha mradi huu.

Je, Serikali sasa iko tayari kukamilisha mradi huu ili mradi adha tuliyonayo pale tuweze kuondokana nayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Butondo, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, yeye mwenyewe kama Mwenyekiti wa Mfuko wa Jimbo kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki, wananchi wake wa Kishapu pamoja na mdau ambaye ni Mgodi wa Almasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imekuwa ikiunga mkono juhudi kama hizi ambazo wananchi wameji-*commit* na nimhakikihsie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kwa sababu tumeshaongea na Mheshimiwa Mbunge kwenye mwaka wa fedha sasa unaoanza 2025/2026 tunatenga fedha kwa ajili ya kumalizia Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kishapu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo la Kibamba tunatoa shukrani sana kwa Serikali kupitia Kituo chetu cha Polisi cha Wilaya ya Chagogoni, kinaendelea kufanya kazi vizuri sana, lakini ni ukweli Jimbo la Kibamba liko pembezoni sana mwa Dar es Salaam na lina idadi kubwa sana ya watu. Sasa eneo la kusini ambao ni King'azi A, King'azi B, Mpakani, Kwa Unju, Saranga na Mtaa wa Ukombozi, ina zaidi ya watu 300,000 na hamna kituo chochote cha polisi cha kuwasaidia usalama nae neo tayari wanalo.

Je, Serikali mnaweza mkaweka *commitment* ya kutusaidia pale kwa ujenzi wa haraka ili wananchi wapate usalama wao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tayari wameshatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha polisi. Sisi kama Serikali tunachuku eneo hilo, tunaliingiza kwenye mpango na tayari kwa kutengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha polisi kwenye eneo ambalo lina watu zaidi ya 300,000 kwa ajili ya usalama wao na mali zao, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nyumba za askari polisi katika Jimbo la Muhambwe ni chakavu sana.

Je, ni lini Serikali itajenga au kukarabati zile nyumba ambazo ni chakavu sana ili kuweka mazingira safi kwa askari wetu wa Jimbo la Muhambwe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Samizi, Mbunge wa Muhambwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Polisi itafanya tathmini katika maeneo yote ikiwemo na Wilaya ya Muhambwe ili kuona kwamba je, nyumba hizo zinafaa kujengwa au kukarabatiwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nyumba zako za

askari katika eneo la Muhambwe pia tutalichukua, tutafanya tathmini na kuingiza kwenye mpango tayari kwa ajili ya ukarabati au ujenzi kutokana na hali tutakayoikuta, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Ifikapo tarehe 15 mwezi ujao, Wilaya ya Liwale inafikisha miaka 50 lakini haijawahi kuwa na jengo la kituo cha polisi. Ni nini mpango wa Serikali kujenga kituo cha polisi ili wananchi wale wasiendelee kupanga? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambaye swali hili ameshauliza mara nyingi na nimeshamjibu, lakini nimhakikishie Serikali hii sikivu ya Dkt. Samia Suluhu Hassan inajua ukosefu wa kutokuwa na kituo cha polisi katika Wilaya ya Liwale na iko tayari imeshawekwa kwenye mpango na itatengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho ili kuhudumia wananchi na mali zao, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako. Bado una swali moja. Nimwite Mheshimiwa Mustafa Mwinyikondo Rajab, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Haji Amour Haji.

Na. 560

**Hitaji la Magari ya Polisi Wilaya ya Magharibi B**

**MHE. HAJI AMOUR HAJI K.n.y. MHE. MUSTAFA MWINYIKONDO RAJAB** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka magari katika Vituo vya Polisi Wilaya ya Magharibi B?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Mei, 2025 Serikali imepeleka gari jipya aina ya *Toyota Land Cruiser Pickup* kwa Wilaya ya Magharibi B Unguja na kufanya wilaya hiyo kuwa na magari mawili sasa. Serikali itaendelea kutenga fedha toka kwenye bajeti yake kila mwaka kwa ajili ya kununua magari na vitendea kazi vingine kwa matumizi ya Jeshi la Polisi na kugawa katika mikoa na wilaya zote hapa nchini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haji.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kajibu vizuri lakini pia vilevile Wilaya ya Magharibi pamoja na kwamba kuna magari mawili ambayo yamepelekwa pale, lakini bado kuna vituo kama Kituo cha Kijitoupele ambacho kiko katika ndani ya Jimbo la Pangawe, kile kituo kina shida sana kwa sababu kina mkusanyiko wa mambo mengi mno.

Sasa sijui ni lini pamoja na kwamba kuna magari, lakini kwamba Serikali itaipelekea angalau zile pikipiki kwa kuweza kufanya *patrol* hasa kwa wakati ule wa kipindi cha uchaguzi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Haji Amour Haji, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali ilishapeleka pikipiki zaidi ya 105 katika kata na shehia kwa upande wa Zanzibar na kwa sababu ametaja suala la uchaguzi, nikuhakikishie Serikali kupitia Jeshi la Polisi tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba maeneo yote yatakuwa salama, lakini pia tutaangalia namna ya kupekeka pikipiki katika eneo hilo ili kusaidia doria na kulinda usalama wa raia na mali zao katika eneo hilo, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Grace Tendega uliuliza swali lakini, haya uliza swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Kituo cha Polisi cha Tanangozi kina changamoto kubwa sana ya gari, lakini Waziri, Mheshimiwa Masauni aliahidi kupeleka samani pale katika kituo kile. Je, ni lini Serikali itapeleka samani na kuwapatia gari? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace Tendega, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali imeshasambaza magari kwa ajili ya ma-*OCD* wilaya zote hapa nchini na ifikapo mwezi Agosti tutakuwa tumesambaza pia magari kwa ma-*OCD* nchi nzima. Kwa hiyo, naamini magari yote haya mawili yakipatikana yatasaidia hapo katika eneo alilotaja Mheshimiwa Mbunge katika eneo lake la Tanangozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu samani tumechukua pia kituo hicho tuingize kwenye mpango tayari kwa kutengewa fedha kwa ajili ya kuipatia samani ili ofisi iendelee kufanya kazi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge siku ya leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza maswali yaliyokuwa kwenye orodha ya shughuli za leo na muda wetu wa maswali tumeumaliza na tumeongeza kidogo.

Sasa nilete wageni ambao tunao katika ukumbi wetu wa Bunge. Kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Tuna wageni 70 wa Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Hawa ni wanafunzi na

walimu wa Shule ya Sekondari Juhudi kutoka Ukonga Dar es Salaam, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 50 wa Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini ambaye ni Naibu wetu Waziri wa Katiba na Sheria. Hawa ni wageni kutoka Chama cha Walimu kutoka Butiama, Mkoa wa Mara. Wako pale, karibuni sana kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Tuna wageni 16 wa Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, hawa ni Chama cha Walimu kutoka Wilaya ya Kwimba, Mkoa wa Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Haya, tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, hawa ni kaka zake kutoka Mkoa wa Geita. Wako wapi? Hatuwaoni lakini labda hawako upande huu, karibuni sana.

Halafu tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, hawa ni familia yake kutoka Jijini Mbeya, karibuni sana kwenye ukumbi wetu wa Bunge. *(Makofi)*

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, hawa ni Watumishi wa Mungu wa Kanisa la KKKT Usharika wa Kisasa na *Nations Prayer Warriors to Project* kutoka Mjini Dodoma. Wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; hawa ni wanafunzi 85 na walimu 11 wa Shule ya Msingi *Mother of Mercy* kutoka Jijini Dar es Salaam. Simameni tuwaone na karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 50 wa Chama cha Skauti wa Shule ya Msingi Matre Dei kutoka Wilaya ya Temeke, Jijini Dar es Salaam. Wako pale na karibuni sana Maskauti. *(Makofi)*

Tuna vijana saba wa Chama cha Skauti kutoka Jijini Dodoma. Maskauti saba wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 65 na walimu 13 wa Shule ya Msingi Brookside kutoka Jijini Dar es Salaam. Wako hapo, karibuni sana kwa mafunzo. *(Makofi)*

Tuna Ndugu Abby Sanga kutoka Jijini Dar es Salaam. Tulimtangaza kabla huyu Abby Sanga.

Waheshimiwa Wabunge, haya ndiyo majina tuliyonayo ya wageni wetu kwa sasa.

Waheshimiwa Wabunge, hakuna matangazo mengine yaliyopo hapa na Bunge sasa litakwenda kwenye shughuli nyingine za Kamati ambazo zitakuwa zinaendelea nje ya Bunge.

Kwa hiyo, sasa ninaahirisha kikao hiki cha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 5.06 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 11 Juni, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*